BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.gp.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU RIPOTI YA TANO YA UTEKELEZAJI WA KAZI ZA TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA ZANZIBAR KWA MWAKA 2020 - 2021

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma, Muumba wa mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake kwa kutujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kufika ndani ya Baraza hili siku ya leo na kuweza kutekeleza majukumu yetu ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, vile vile, nitumie fursa hii kukutakia kheri na siha njema wewe binafsi Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu kwa ajili kutoa maoni ya Kamati yetu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu uwasilishwaji wa Ripoti ya **Utekelezaji wa Kazi za Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa Mwaka wa fedha 2020/2021.**

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa nafasi hii napenda kumshukuru na kumpongeza Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Mheshimiwa Haroun Ali Suleiman, kwa kuwasilisha kwa uweledi wa hali ya juu mbele ya Baraza hili Ripoti ya tano ya Utekelezaji wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa kipindi cha mwaka 2020/2021. Ripoti hii inaonesha wazi jinsi Tume inavyotekeleza vyema majukumu yake nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa sasa naomba niwatambue kwa majina Wajumbe wa Kamati yangu kama ifuatavyo:

	Mhe. Hassan Khamis Hafidh	Mwenyekiti
2.	Mhe. Mtumwa Peya Yussuf	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Machano Ohman Said	Mjumbe
4.	Mhe. Zaina Abdalla Salum	Mjumbe
5.	Mhe. Suleiman Makame Ali	Mjumbe
6.	Mhe. Salma Mussa Bilal	Mjumbe
7.	Mhe. Mohammed Mgaza Jecha	Mjumbe
8.	Ndg. Ali Alawy Ali	Katibu
9.	Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir	Katibu
10.	Ndg. Amina Abeid Hemed	Mkalimani

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa na kwa niaba ya Kamati napenda kuwapongeza viongozi na watendaji wote wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Asaa Rashid kwa kazi zao wanazozifanya zenye dhamira ya kuhakikisha kuwa tabia na vitendo vyenye kufuata maadili kwa viongozi wa umma vinavyoimarisha uwajibikaji, utii na usimamizi wa sheria zinatekelezeka ipasavyo licha ya kuwa Tume hii inakumbana na changamoto mbalimbali.

Mheshmiwa Spika, baada ya utangulizi huo, sasa naomba kwa niaba ya Mwenyekiti kutoa maoni ya Kamati yangu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusiana na Ripoti ya Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza sana Tume kwa kuweza kutayarisha na kuileta mbele ya Baraza hili kwa ajili ya kuiwasilisha ripoti yao hii kwa mara ya tano mfululizo tokea kuanzishwa kwake kama ilivyoelekezwa katika kifungu cha 29(1) na (2) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam.4 ya 2015. Hii inadhihirisha wazi ni kiasi gani utendaji kazi wa Tume ya Maaadili unazingatia misingi ya maadili, utaalamu na uadilifu wa hali juu.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Kamati imeridhika na Ripoti ya Utekelezaji wa Kazi za Tume ya Maadili kwa mwaka 2020/2021 kwa kuzingatia malengo na msingi wa kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa kipindi kilichotajwa hapo juu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, katika ukurasa wa 5&6 ambao umeeleza makundi makuu ya viongozi wanaosimamia na kuwajibika na masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Kamati inashauri kupitia kundi la (v) lililotaja viongozi walioainishwa kutokana na unyeti na uzito wa kazi na majukumu yao kuongezwa pia, wasaidizi wahasibu, waweka hazina na maafisa manunuzi kutokana na kuwepo kwa majukumu mazito wanayotekeleza kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa uwasilishaji wa Fomu ya tamko la mali na madeni uliyoelezwa katika uk wa 7&8 kwa kila kiongozi aliyetajwa katika jadweli la kwanza la sheria ya Maadili. Kamati inashauri kuwepo mkakati maalum wa kutoa elimu ya kutosha kwa wajazaji fomu za tamko kwa viongozi wapya wa umma mara tu baada ya kutangazwa na kuapishwa kama ambavyo Sheria inavyoelekeza kwa kiongozi mpya kujaza fomu ndani ya siku 30 baada ya kiongozi wa Umma kushika Madaraka au wadhifa wa uongozi.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inaishauri Tume ya Maadili kutoa taaluma ya kutosha dhidi ya wajazaji fomu kwa kuitumia tovuti yao inayopatikana katika kipengele hichi cha uchapishaji na usambazaji wa fomu ya tamko la Mali na Madeni kwa kupakuwa fomu hizo na kuzijaza badala ya kusubiri kupatiwa kwa barua ili kuweza kurahisisha zoezi hizo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ugumu wa upatikanaji wa fedha Kamati inatoa pongezi za dhati kabisa kwa Tume kuvuka malengo yake katika upokeaji wa fomu kwa wakati. Hata hivyo, kupitia ripoti hii Kamati inawaomba viongozi wote wanaostahili kujaza fomu hizi kukamilisha zoezi ya ujazaji fomu ndani ya mda na kuzirudisha ofisi husika ili kuiwezesha Tume kufanya kazi zake ipasavyo. Kamati inaishauri Tume, kutumia adhabu mbadala kwa wale wote ambao huwasilisha fomu zao nje ya muda. Aidha, Kamati inashauri Mamlaka za uteuzi kuwachukulia hatua kali viongozi ambao wanachelewa kujaza fomu hizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefarijika kuona kuwa Tume ya Maadili imezidi

kuimarisha utendaji wake wa kazi za kupokea na kusajili taarifa mbali mbali zinahusiana na Viongozi wa Umma kwa njia za kielektroniki. Aidha, Kamati inaridhia mpango wa Tume wa kuandaa mfumo wa taarifa za kimaeneo ambao utatoa taarifa za kumbukumbu za viongozi wanaofanyiwa uhakiki katika maeneo ya mali zao. Hata hivyo, Kamati inasisitiza kuwa mfumo huu wa ujazaji taarifa zinazowekwa katika mtandao huo ziwe katika hifadhi salama na zenye kuaminika ili taarifa hizo zisiweze kusambaa kirahisi na kupelekea utekelezaji wake kuwa mgumu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa msisitizo kwa Tume ya Maadili kuwa utaratibu wanaoutumia kuelimisha viongozi wa umma na wananchi juu ya dhana ya utawala bora na misingi yake kupitia maadhimisho ya siku ya Maadili na Haki za Binadamu ambayo kwa kawaida hufanyika kila ifikapo tarehe 10 Disemba ya kila mwaka kwa kuitangaza na kuonesha shamra shamra za wiki ya Maadili kupitia vyombo vya habari na kuzidi kuwahimiza wananchi na viongozi mbali mbali kulinda na kuendeleza maadili mema katika jamii.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia, inaipongeza Tume katika kuwajengea uwezo wafanyakazi wake kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu katika fani mbalimbali. Kamati inashauri Serikali kutotosheka na taaluma za ndani wanazowapatia wafanyakazi hao bali kuwapatia pia mafunzo ya nje ya nchi ili kuongeza uwelewa wa kiwango chao cha kupata elimu zaidi.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya upatikanaji wa fedha za Matumizi Mengineyo (OC) katika Tume ya Maadili jambo ambalo wanashindwa kukamilisha programu zao mbali mbali wanazojipangia. Ikiwa pamoja na Tume inashindwa kutoa elimu ya kutosha kwa viongozi na jamii kwa ujumla kutokana na uhaba wa fedha. Sambamba na hilo, Tume inakabiliwa na uhaba wa vyombo vya usafiri kwa maafisa wake. Hivyo, kushindwa kutekeleza majukumu yao kwa wepesi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kufuatia changamoto hizi zilizojitokeza katika uk wa 21 Kamati inashauri Serikali kuiangalia Tume hii kwa jicho la huruma ili kuisaidia kutimiza majukumu yake kama inavyojipangia pamoja na kuwapatia fursa watendaji wake ya kupata mafunzo ya ndani na nje ya nchi ili kufikia malengo wanayoyakusudia.

Mheshimiwa Spika, vile vile katika suala la kutoa taarifa kuhusiana na tuhuma au malalamiko ya uvunjwaji wa Maadili Kamati inashauri uwepo uchunguzi wa kina na wa haraka wa taarifa zinazowasilishwa na wananchi kabla ya hatua madhubuti kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kukosekana kwa taarifa za uteuzi wa viongozi wanaoteuliwa na Waziri, Tume na Bodi za Wakurugenzi na wengineo ambao hupelekea kuandikiwa barua za kuwasilisha taarifa za uteuzi zinazohusika pamoja na taarifa za mabadiliko, uhamisho au kustaafu kamati inasikitishwa sana na kitendo hicho hivyo, inashauri kufanyika kwa juhudi za makusudi zitazowezesha kupatikana taarifa hizo kiurahisi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inasisitiza kuongezwa kwa watumishi wanaohitajika hasa ofisi za Tume Pemba na kuwapa mafunzo ya kukuza uwezo ili kazi za Tume ziweze kutekelezeka kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa inatoa pongezi zake za dhati kwamara nyengine tena kwa kuweza kuwasilisha ripoti hii kwa wakati Barazani pamoja na kazi nzuri za Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya kuhakikisha inasimamia maadili ya viongozi na imepata mafanikio mengi yenye kukamilisha dira na dhamira ya Tume hii kwa muda mfupi tokea kuanzishwa kwake. Kwa hivyo, lengo kuu lililokusudiwa litafikiwa endapo misingi mikuu ya Maadili itazingatiwa, ambayo ni uadilifu, usiri, utaalamu, uwajibikaji na kufanya kazi kwa mashirikiano.

Mheshimiwa Spika, kamati yetu pia, inatoa pongezi na shukurani za dhati kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa kusisitiza kila wakati kwa viongozi wote wafuate maadili na utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia naomba kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini wakati wote ambao naiwasilisha hotuba hii, na pia nizidi kuwashukuru wajumbe wa Kamati yangu kwa mashirikiano yao makubwa waliyonipatia pamoja na kuwa na msimamo thabit kwa wanacho kisimamia. Aidha, niwaombe wajumbe wa Baraza hili Tukufu kuisoma na kuifahamu vyema ripoti hii ili tuweze kuona mambo mbalimbali yaliyoelezwa ndani yake.

Mheshimiwa Spika, Naomba Kuwasilisha.

.....

Machano Othman Said

Kny: Mwenyekiti,

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

BARAZA LA WAWAKILISHI

ZANZIBAR